

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Wekeza, paliishi familia ya Mzee Akiba. Mzee Akiba na mkewe, Maimuna, ambaye alikuwa mrembo kama hurulaini, walikuwa na watoto wawili walioitwa Liwe na Liwalo. Mzee Akiba alifahamika sana kijijini Wekeza kwa mambo chungu nzima. Alikuwa na uwezo wa kuwahamasisha wanakijiji waanzishe biashara ndogondogo za kuwazalishia mali kochokocho. Yeye binafsi alikuwa kielelezo. Awali alianza na kibanda cha kuuzia mazao aliyoyatoa katika kikataa chake kidogo. Aliendelea polepole na kuibuka kuwa bwanyenye mwenye dukakuu la Malimali ambalo lilifahamika kona zote za kijiji cha Wekeza.

Ungemwuliza Mzee Akiba jinsi alivyojizolea mali yake na kuwa tajiri aliyenuka pesa, angekuambia wimbo ufuatao:

*Kidogo kidogo hujaza kibabaa.*

*Ukipata kidogo usikile chote.*

*Ukipata mbili weka moja, weka mojaa, weka mojaa.*

*Kumbuka akiba haiozangi, haiozangi, haiozangii!*

Akisha kuambia angekupasulia waziwazi kuwa maendeleo yoyote aushini hutokana na mtu kujinyima. Angeeleza kuwa chochote unachokipata lazima utumie kwa kipimo na kuweka kidogo cha kukufaa kwa hali na mali kwa siku za halafu. Ungemdadisi zaidi angekuuliza, “Hebu nionyeshe mtu yeyote hapa Wekeza aliyeulalia umaskini na kuuamkia utajiri! Yuko wapi? Hakunaa! Hakuna nakwambia!” angesisitiza. Angekukumbusha kuwa kidogo kidogo ndicho hujaza kibaba hatimaye! Naam, hicho ndicho kisa cha Mzee Akiba na jinsi alivyoinuka maishani. Kwa kweli, akiba haiozi.